

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA Uvaaji wa Barakoa Shuleni

New Brunswick
Nouveau Brunswick



Barakoa ya kitambaa ni nini?

Barakoa yenye angalau safu mbili za vitambaa zilizoshonwa pamoja. Inapaswa kumfanya mtu ajihihi vizuri anapoivaa na iwe kubwa kiasi cha kuziba pua, mdomo, na pande za uso wa mtoto/watoto wako. Haipaswi kuwa na michaniko na matobo na inapaswa kumwezesha mtoto wako kupumua vizuri.



Mtoto wangu aende na barakoa ngapi shuleni kila siku?

Tunapendekeza kwamba kila mwanafunzi aje shuleni na barakoa mbili zilizo safi kila siku. Kuwa na barakoa mbili humwezesha mtoto wako kuwa na nyingine ya akiba ikitokea moja imechafuka.



Mtoto wangu anapaswa kuvuaja barakoa?

Kabla ya kuvua barakoa, mtoto wako anapaswa kunawa mikono yake kwa sabuni na maji ya uvuguvugu au kutumia kitakasa mikono.

Barakoa inaweza kuvuliwa kwa kulegeza kamba au kuondoa mipira kwenye masikio. Ikiwa barakoa inalazimu kuvaliwa zaidi ya mara moja wakati wa mchana, inaweza kushikwa kwenye mipira au kamba na kisha kuweka kwenye mfuko wa kuhifadhia vitu au kikasha kwa matumizi ya baadaye. Ikiwa barakoa inahitaji kufuliwa, inaweza kuwekwa kwenye mfuko au kikasha cha kuhifadhia vitu kilichowekwa alama kwa dhumuni hili ili iweze kupelekwa nyumbani kwa ajili ya kufuliwa.



Napaswaje kuzitunza barakoa za mtoto wangu?

Barakoa inapopata unyevu, inapaswa kuvuliwa na kuwekwa kwenye mfuko ulioandikwa barakoa zilizotumika au zilzochafuka. Barakoa zilizotumika zinapaswa kufuliwa kila siku kwenye maji ya moto na sabuni na kuachwa zikauke kabla ya kuvaliwa tena.

Barakoa haipaswi kuning'inia kwenye shingo au masikio ya mtoto wako. Haipaswi pia kuvaliwa chini ya pua au kidevu.

Unaweza kumkumbusha mtoto wako kutoigawa barakoa yake na kutoigusa wakati akiwa ameivaa. Wakati ambapo barakoa haivaliwi shuleni, inapaswa kuwekwa kwenye mfuko wa plastiki au kikasha cha kuhifadhia vitu.



Mtoto wangu anapaswa kuvaaje barakoa?

Kabla ya kuvaa barakoa, mtoto wako anapaswa kunawa mikono kwa sabuni na maji ya uvuguvugu au kutumia kitakasa mikono.

Barakoa inapaswa kukunjuliwa kabisa na kisha kuwekwa kwenye pua, mdomo na kidevu na kufungwa kwa kamba au mipira ya masikioni. Ikiwa kuna kisaidizi cha pua, kinaweza kufinywa sehemu ya pua kwa ulinganifu mzuri ili kusiwe na nafasi kati ya sura na barakoa.



Mtoto wangu azihifadhi vipi barakoa wakati hazitumiki?

Barakoa zinaweza kuhifadhiwa kwenye mifuko ya plastiki au vikasha vya kuhifadhia vitu, kwenye begi la mgongoni la mtoto wako. Barakoa zilizotumika au zilzochafuka zinaweza kuhifadhiwa kwenye mfuko tofauti wa plastiki au kikasha tofauti cha kuhifadhia vitu. Unaweza kuweka alama kwenye mfuko au kikasha ili mtoto ajue mahali pa kuweka barakoa zilizotumika ambazo zinapaswa kufuliwa. Ni wazo zuri kuandika jina la mtoto wako kwenye barakoa ili zisitumiwe kwa bahati mbaya na watoto wengine.